USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

PELUM ASSOCIATION

# HAKI ZA ARDHI KWA WANAWAKE



# Haki za Ardhi kwa Wanawake

*Kitini hiki cha Haki za Ardhi kwa Wanawake Tanzania kimeandaliwa na PELUM Tanzania kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Maendeleo la Msaada la Watu wa Marekani (USAID). PELUM Tanzania inawajibika kwa maudhui yaliyomo ndani ya kitini hiki na maudhui hayo hayawakilishi msimamo wa USAID au Serikali ya Marekani.*

**Haki za Ardhi kwa Wanawake**

© PELUM Tanzania 2015

ISBN 978-9987-8956-8-7

Mchora Katuni: Godwin J. Chipenya

**Kwa mawasiliano zaidi:**
Mratibu,
PELU M Tanzania
S.L.P 390, Morogoro-Tanzania
Simu/Nukushi: +255 23 2613677
Barua pepe: info@pelumtanzania.org
Tovuti: www.pelumtanzania.org

# YALIYOMO


Shukrani 1

Utangulizi 2

**Sura ya Kwanza** **3**

Sheria za Ardhi na Nafasi ya Mwanamke katika Kumiliki Ardhi 3
Maana ya Ardhi 3
Sheria Zinazosimamia Masuala ya Ardhi na Jinsia kwa Ujumla 3
Nafasi na Haki ya Mwanamke katika Kumiliki Ardhi 5
Umiliki wa Ardhi Chini ya Sheria ya Ardhi 6
Rehani katika Ardhi 8
Hitimisho 10

**Sura ya Pili** **11**
***Sehemu ya Kwanza*** ***11***

Sheria ya Ndoa na Haki ya Ardhi kwa Mwanamke 11
Maana ya Ndoa 11
Aina za Ndoa 11
Dhana ya Kuchukulia/Ndoa za Kufikiria 13
Haki na Wajibu katika Ndoa 14
Haki ya Ardhi ya Mwanamke Wakati wa Talaka 15
Kutengana kwa Talaka 16
Sababu za Mahakama kutoa Talaka 16

***Sehemu ya Pili*** ***17***

Mambo ya Msingi katika Urithi wa Mali ya Familia 17
Maana ya Mirathi 17
Sheria za Kimila 17
Mjane 19
Mjane Asiye na Mtoto 19
Sheria ya Kiislamu 20
Sheria ya Serikali 21
Mahali pa Kufungulia Kesi za Mirathi 22

***Sehemu ya Tatu*** **22**

Wosia 22

Wosia katika Sheria za Kimila 24

Wosia katika Sheria za Kiserikali 24

Wosia katika Sheria ya Kiislamu 24

Namna ya Kuhifadhi Wosia 24

Taratibu za Kufungua Mirathi 25

Hitimisho 26

**Sura ya Tatu** **27**

Ushiriki wa Wanawake katika Masuala ya Ardhi 27

Baraza la Taifa la Ushauri la Ardhi 27

Kamati ya Uamuzi ya Kijiji 27

Baraza la Kata 28

Baraza la Ardhi la Kijiji 28

Hitimisho 28

# SHUKRANI

Kitini cha **Haki za Ardhi kwa Wanawake** kimeandaliwa na shirika la PELUM Tanzania kwa ufadhili kutoka shirika la Maendeleo la Msaada la Watu wa Marekani (USAID) kupitia Mradi wa Ushiriki wa wananchi katika kusimamia sekta ya kilimo (Citizen Engaging in Government Oversight in Agriculture) unaolenga kuhusisha ushiriki wa wananchi katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za serikali pamoja na uwajibikaji wa serikali kwa ujumla katika masuala ya ardhi.

Kitini hiki kinalenga kuelimisha jamii juu ya sheria mbalimbali zinazomgusa mwanamke hasa katika upatikanaji, umiliki, na utumiaji wa ardhi. Vilevile ni nyenzo ya kuamsha uelewa wa wanajamii hasa waishio vijijini juu ya masuala mbalimbali ya haki za ardhi kwa mwanamke ukizingatia kwa sasa kuna changamoto kubwa katika jamii juu ya uelewa kuhusu sheria zinazogusa haki za ardhi za wanawake.

Shukrani za dhati ziende kwa Mashirika ya Uluguru Mountains Agricultural Development Project (UMADEP), Tanzania Grass Roots Oriented Development (TAGRODE), Institut Africain pour le Développement Economique et Social (INADES FORMATION TANZANIA) HAKIARDHI, Lawyers' Environmental Action Team ( LEAT) na Naramatishe Pastoralists Society Organisation (NAPASO) ambayo yalihusika katika kuboresha Kitini hiki.

Shukrani pia ziende kwa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) kwa mchango wao katika kuhakikisha kuwa Kitini hiki kinakua na kiswahili fasaha. Tunashukuru pia Halmashauri zote za wilaya ya Bahi, Kongwa, Kilolo, Mufindi, Mvomero na Morogoro ambazo zilihusika kukiboresha kitini hiki ili kiwe na maudhui sahihi kwa wasomaji.Shukrani za pekee ziende kwa shirika la maendeleo la watu watu wa Marekani kwa kufadhili kitini hiki. Pia, shukrani ziende kwa shirika la PELUM Tanzania mradi wa CEGO kwa uaandaji na uchapishaji wa kitini hiki. Tunaamini kuwa kitini hiki kitakuza na kitaongeza uelewa wa sheria zinazogusa haki za ardhi za wanawake na kumuweka mwanamke katika nafasi sawa sawa na mwanaume katika kutumia, kumiliki na kuitunza ardhi. Hivyo kuifanya jamii (hasa wazalishaji wadogo) kufikia maendeleo endelevu katika nyanja zote za maisha kwa kutambua mchango wa mwanamke katika kukuza kilimo endelevu.

# UTANGULIZI

Ardhi kama rasilimali muhimu inayotumiwa na wakulima wadogo na watu mbalimbali hapa nchini ina umuhimu mkubwa sana katika mai-sha ya binadamu, wanyama, mimea na viumbe vyote. Ardhi ni mion-goni mwa rasilimali za msingi katika uhai na maendeleo ya binadamu, wanyama na mimea.

Ardhi ni rasilimali muhimu ambayo kila mwananchi anaihitaji katika kuendeleza maisha yake. Aidha ni rasilimali inayohitajika pia ili kuen-deleza sekta nyingine za uchumi kama vile kilimo, viwanda, biashara na uwekezaji. Hivyo basi, ardhi ni hitaji la muhimu na pia ni haki ya kila binadamu (mwanaume na mwanamke) kuimiliki, kuitumia na kutunza ardhi kwa mujibu wa sheria ya Tanzania.

Kwa muda mrefu sasa mila na desturi nyingi katika nchi yetu Tanzania zimekuwa zikimnyima mwanamke haki ya kumiliki ardhi, ukilinganisha na mwanaume. Mwanamke amekuwa ndiye mtumiaji mkuu wa ardhi lakini hanufaiki na pato linalopatikana kutokana na nguvu zake juu ya ardhi hiyo.

Kitini hiki kinalenga kuelezea haki mbalimbali alizonazo mwanamke katika ardhi kwa mujibu wa sheria za nchi ya Tanzania. Pia, kitaelezea namna mwanamke anavyoweza kunufaika na ardhi anayoitumia kwa ajili ya maendeleo yake, familia na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Maendeleo hayo yanajumuisha matumizi ya ardhi yanayozingatia ma-hitaji ya kizazi kilichopo bila kuathiri mahitaji ya vizazi vijavyo.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 SHERIA ZA ARDHI NA NAFASI YA MWANAMKE KATIKA KUMILIKI ARDHI

### 1.1 MAANA YA ARDHI

Ardhi kwa mujibu wa kifungu cha 2 cha Sheria ya Ardhi Namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 za mwaka 1999, ni ile inayojumuisha vitu vyote vilivyo juu na chini ya uso wa nchi vikiwemo majengo, uoto wa asili na maendelezo yote yaliyofanywa au yanayofanywa isipokuwa madini, petroli na gesi.

### 1.2 SHERIA ZINAZOSIMAMIA MASUALA YA ARDHI NA JINSIA KWA UJUMLA

Masuala ya ardhi na jinsia kwa Tanzania yanasimamiwa na sheria mbalimbali kama zifuatazo:-

- Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977
- Sheria ya Ardhi Namba 4 ya 1999
- Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya 1999
- Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Namba 2 ya 2002
- Marekebisho ya sheria ya Ardhi Namba 2 ya 2004
- Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971
- Marekebisho ya sheria Namba 11 ya 2005 sehemu ya nne

Kitini hiki kimejikita zaidi katika sheria za ardhi na sheria zingine zinazohusika katika kusimamia ardhi na jinsia, zaidi ya hayo, kimeangalia nafasi ya mwanamke katika kupata, kutumia na kumiliki ardhi Tanzania.

#### 1.2.1 KATIBA YA JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA YA MWAKA 1977

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama sheria mama inasisitiza kwamba, binadamu wote ni sawa na huzaliwa huru hivyo basi, wanatakiwa kupata ulinzi sawa wa Sheria za nchi. Kwa maana hiyo mwanaume na mwanamke wanahaki sawa mbele ya sheria na wanatakiwa kupewa ulinzi sawa na Sheria za nchi ikiwemo kumiliki, kutumia na kupata ardhi kwa mahitaji yao. Kwa kuwa kila mtu anayo haki ya kumiliki mali, na haki ya hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa

mujibu wa Sheria. Hivyo, mwanamke ana haki ya kumiliki ardhi kama mojawapo ya mali na kupata ulinzi wa mali hiyo kulingana na Katiba ya nchi.

Kwa maelezo hayo, ni wazi kwamba, suala la kumiliki na kutumia ardhi kwa mwanamke na mwanaume kwa usawa ni la kikatiba. Kwa upande mwingine mwanaume anatakiwa kulinda mali hiyo na kulinda mali ya mtu mwingine inayomilikiwa mwanamke kihalali na kwa taratibu za Sheria.

### 1.2.2 SHERIA ZA ARDHI

Sheria ya Ardhi Namba 4 na Sheria ya ardhi ya Vijiji Namba 5 zimetungwa kutokana na Sera ya Ardhi ya Taifa ya mwaka 1995 inayolenga kulinda rasilimali ardhi katika kuwawezesha wananchi kupata, kutumia na kumiliki ardhi nchini. Sheria hizi pia zimeeleza jinsi gani mwanamke kama mtumiaji ardhi anaweza kupata na kunufaika na rasilimali hii. Sheria hizi zimetungwa ili kuweka bayana masuala ya umiliki wa ardhi hususani kuondoa tofauti zilizopo katika kufanya maamuzi yanayohusiana na masuala ya ardhi kwa wanawake.

Sheria hizi, zimezingatia msingi wa usawa na haki katika kumiliki ardhi, pia zimeeleza bayana kuwa, haki ya kila mwanamke kupata, kumiliki na kutumia ardhi, itakuwa sawa sawa na kwa masharti yaleyale kama ilivyo kwa mwanaume. Sheria pia, zimeondoa ubaguzi dhidi ya wanawake. Mwanamke anayetaka ardhi, atafuata taratibu zote zinazohusika, na hapaswi kunyimwa ardhi kwa sababu tu yeye ni mwanamke. Hivyo Sheria hizi zinaonesha wazi kuwa hakutakuwa na tofauti yoyote katika haki juu ya masuala ya ardhi kwa jinsi zote.

### 1.3 MISINGI MIKUU YA SHERIA ZA ARDHI

Sheria za ardhi  zimeweka misingi mikuu katika ardhi kuwa ardhi ni mali ya umma na imekabidhiwa kwa Rais kwa niaba ya Watanzania wote, hivyo  raia wote wanawake na wanaume wana haki sawa ya kupata, kumiliki, kutumia na kuuza ardhi.

Pia imebainisha milki za ardhi zilizopo ikiwa ni pamoja na milki ya kimila na ile ya hati  zinazotambuliwa  na kulindwa kisheria ,aidha fidia kamili na ya haki ilipwe kwa mmiliki wa ardhi  bila kuchelewa pale ardhi yake inapotwaliwa na serikali kwa ajili ya manufaa ya umma.

Sheria pia imesisitiza kwamba ardhi itumike kwa manufaa yanayozingatia maendeleo endelevu, na kuwepo na mfumo bora wa utawala na usimamizi wa ardhi ambao unawawezesha wananchi kushiriki katika kufanya maamuzi kuhusu masuala ya ardhi wanayokalia na kutumia.

**1.4 NAFASI NA HAKI YA MWANAMKE KATIKA KUMILIKI ARDHI**

Sheria hizi za ardhi, Sheria ya Ardhi Namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 za mwaka 1999 zimebainisha nafasi na haki mbali mbali alizonazo mwanamke katika ardhi, haki hizo ni pamoja na kupata, kutumia, kumiliki na kuuza ardhi. Mwanamke kwa mujibu wa sheria ana haki ya kuomba ardhi na kupewa sawa sawa na haki aliyonayo mwanaume. Katika ngazi ya kijiji, Halmashauri ya Kijiji inatakiwa kuzingatia usawa wa watu wote, kama vile kuyapa uamuzi sawa maombi toka kwa mwanamke au kikundi cha wanawake na yale yanayotoka kwa mwanaume au kikundi cha wanaume. Yaani kutokuwa na ubaguzi wowote dhidi ya mwanamke aliyeomba kupewa ardhi kwa hakimiliki ya kimila. Uamuzi wowote wa Halmashauri ya Kijiji au chombo chochote kinachoshughulikia ardhi utakuwa batili iwapo uamuzi huo utawanyima wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu haki za ardhi kisheria.

**1.5 NAFASI YA MWANAMKE KATIKA KUMILIKI ARDHI YA KIJIJI**

Sheria ya ardhi Namba 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 zimetambua aina kuu mbili za milki ya ardhi ya kimila na ya hati. Ambapo milki ya kimila inatumika katika ardhi ya kijiji na ya hati inatumika katika ardhi ya kawaida ambayo mara nyingi ni ardhi iliyopimwa na inapatikana maeneo ya mjini na maeneo baadhi ya vijijini ambayo hayakaliwi wala kutumiwa na wanakijiji.

Sheria ya ardhi Namba 4 ya mwaka 1999 imeigawa ardhi katika makundi makuu matatu:

i. **Ardhi ya kawaida,** hii ni ardhi yote ya umma ambayo siyo ardhi ya hifadhi wala ardhi ya kijiji. Hata hivyo, ardhi ya jumla inajumuisha pia ardhi ya kijiji ambayo, haikaliwi wala kutumiwa na wanakijiji. Kamishna wa ardhi ndiye msimamizi wa kundi hili la ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi namba 4 .

ii. **Ardhi ya hifadhi,** hii ni ardhi iliyotengwa kwa shughuli

maalum na kuwa chini ya usimamizi wa mamlaka husika kama vile hifadhi ya misitu,  mikoko na matumbawe, ardhi oevu, visiwa vilivyopo karibu na fukwe za bahari au maziwa, ardhi inayotumiwa kutupa taka zenye sumu, ardhi yote iliyo ndani ya meta 60 kutoka ukingo wa mto au ziwa, ardhi yenye miteremko mikali, hifadhi za taifa, vyanzo vya maji, barabara, ardhi yenye madhara na  n.k

**iii. Ardhi ya kijiji;** hii ni ardhi ambayo ipo ndani ya mipaka ya eneo la kijiji. Ardhi ya kijiji inajumuisha ardhi yote iliyomo ndani ya mipaka ya vijiji vilivyosajiliwa, ambapo Halmashauri ya kijiji na Mkutano mkuu wa kijiji vimepewa mamlaka ya kusimamia.

Katika ardhi ya kijiji mwanamke amepewa haki kisheria ya kumiliki ardhi ya kijiji, mwanamke anaweza kuomba ardhi kwa kupeleka maombi yake katika halmshauri ya kijiji na kisha kuidhinishwa na mkutano mkuu wa kijiji. Halmashauri ya Kijiji inatakiwa kuzingatia usawa kwa, mwanamke na mwanume.

Katika kuhakikisha nafasi ya mwanamke kumiliki ardhi ya kijiji, kifungu cha 3(2) cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji, kinaeleza wazi kuwa haki ya kila mwanamke katika kupata, kutumia, na kugawa ardhi itakuwa sawa na kwa masharti yale yale kama ilivyo haki ya mwanaume. Sheria hii inaeleza kwamba hakutakuwa na tofauti yoyote katika haki juu ya masuala ya ardhi kwa jinsi zote.

## 1.6 UMILIKI WA ARDHI CHINI YA SHERIA YA ARDHI

Kuna aina mbili za umiliki wa ardhi:

*i. Umiliki wa mtu binafsi*

*ii. Umiliki wa pamoja*

Umiliki wa mtu binafsi:  sheria inatoa nafasi na haki kwa mwanamke au mtu mwingine yeyote kuomba na kumiliki ardhi yake yeye binafsi, hata kama ameolewa.

Umiliki wa pamoja: Huu ni umiliki wa zaidi ya mtu mmoja. Umiliki huu wa pamoja uko wa aina mbalimbali:-

i. Umiliki wa pamoja wa hisa zinazogawanyika

ii. Umiliki wa pamoja wa hisa/maslahi isiyogawanyika.

Umiliki wa pamoja wa hisa zinazogawanyika. Chini ya umiliki huu,

endapo mmiliki mmoja atafariki basi hisa zake zitahamia kwa warithi wake.

Umiliki wa pamoja wa hisa zisizogawanyika. Sheria imeweka bayana kuwa, umiliki wa aina hii unatolewa kwa idhini ya mahakama kuu tu. Chini ya umiliki huu, endapo mmiliki mmoja atafariki basi hisa zake zitahamia kwa wamiliki au mmiliki aliyebaki. Hii ina maana ya kuwa mmiliki mmoja akifariki hisa zake zinaenda kwa wamiliki au mmiliki aliyebaki, warithi wa marehemu hawana haki ya kurithi bali mmiliki wa mwisho atakayekua amebaki.

Katika umiliki wa pamoja wa aina yoyote ile ni lazima majina ya wamiliki wote yawepo kwenye hakimiliki na kila mmoja awe na nakala ya hakimiliki. Sheria inaeleza bayana kuwa wanandoa wanaweza kuomba hakimiliki ya ardhi kwa pamoja katika maslahi/mafungu yanayogawanyika au yasiyogawanyika.

Hakuna mmiliki anayeruhusiwa kuuza, kugawa, kuhamisha, kubadilisha umiliki au kuweka rehani ardhi ila ni **lazima** kwanza awashirikishe wamiliki wote na watoe ridhaa zao kwa maandishi. Sheria pia inaruhusu mwanandoa kumiliki ardhi binafsi au kumiliki kwa pamoja ila ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

- Mwanandoa mmoja anapoomba hakimiliki ya ardhi atatakiwa kueleza bayana kama anachukua hakimiliki hiyo kwa ajili yake binafsi au kwa ajili ya familia katika hakimiliki ya pamoja kwa maslahi/mafungu yasiyo gawanyika. Endapo jambo hili halitawekwa bayana na hakimiliki imechukuliwa kwa umiliki wa pamoja baina ya wanandoa basi, kutakuwepo na dhana ya kuwa wanandoa wote wanamiliki ardhi hiyo kwa maslahi/mafungu yanayogawanyika, na msajili wa hati atatakiwa kuwaandikisha wanandoa hao umiliki wa pamoja wa maslahi/mafungu yanayogawanyika. Inapotokea kwamba mwanandoa anamiliki ardhi au nyumba kwa jina lake Mwenyewe, na mwanandoa mwenzie amechangia nguvu zake katika kuitunza au kuiendeleza nyumba au ardhi hiyo, mwanandoa aliyechangia ana haki pia ya umiliki wa nyumba hiyo.

**Angalizo:** Sheria imeweka bayana kwamba umiliki wa pamoja wa hisa zisizogawanyika utakaochukuliwa bila kibali cha mahakama ni ule wa mke na mume. Watu wengine wote watakaopenda kumiliki ardhi chini

ya umiliki wa ardhi wa pamoja wa hisa isiyogawanyika watalazimika kwanza kupata kibali cha mahakama.

## 1.7 REHANI KATIKA ARDHI

Rehani ni dhamana ya mkopo. Mmiliki wa ardhi anaweza kuomba mkopo kwa kuweka ardhi yake kama dhamana ya mkopo aliochukua katika taasisi yoyote ya kifedha.

Sheria ya Ardhi inampa haki mmiliki wa ardhi kuweka rehani ardhi au nyumba anayomiliki kwa ajili ya kupata mkopo. Hata hivyo kuweka rehani ardhi au nyumba inayomilikiwa na wanandao **lazima** kwanza ipatikane ridhaa ya wanandoa wote wanaoishi au kutumia ardhi hiyo. Hivyo maombi ya rehani yanatakiwa kujazwa katika fomu maalumu na kuwekwa saini na wanandoa wote.

Ni wajibu wa mkopaji kumhakikishia mtoa mkopo kwamba nyumba au ardhi inayowekwa rehani siyo ya familia au ni ya familia, kama ni ya familia basi mwenza wake ameridhia, na kama mkopaji amedanganya atatakiwa kulipa faini ya nusu ya mkopo aliochukua.

### 1.7.1 REHANI YA KIMILA

Rehani ya kimila itafuata taratibu za kimila zinazotumika katika eneo hilo. Hata hivyo, kama kuna tatizo lolote juu ya rehani wahusika watatakiwa kutumia huduma ya Baraza la ardhi la Kijiji.  Baraza la ardhi la kijiji litatakiwa kuangalia kama rehani ilikuwa na masharti yanayozingatia haki na taratibu za rehani ya kimila katika eneo husika.

Kama mkopeshwaji amekiuka masharti ya mkataba wa rehani mkopeshaji anatakiwa ampe taarifa mkopeshwaji kumjulisha ukiukwaji huo na kumtaka arekebishe tatizo hilo. Endapo mkopeshwaji atashindwa kurekebisha tatizo hilo ndani ya muda wa siku thelathini (30) tangu kutolewa kwa taarifa (notice) hiyo, Mkopeshaji anaweza kuuza ardhi au nyumba iliyowekwa rehani.

Ieleweke wazi kuwa hata kama mkopeshwaji atakuwa amekiuka masharti ya rehani mkopeshaji haruhusiwi kuchukua na kumiliki ardhi inayotumiwa na mkopaji kwa ajili ya kilimo au ufugaji au kuingia na kuishi ndani ya nyumba iliyowekwa rehani endapo nyumba hiyo ndiyo makazi ya mkopeshwaji au ndugu wa mkopeshwaji. Mkopeshaji

anaweza kufanya hivyo tu kwa kupata kibali cha mahakama.

***Utaratibu wa kufuata pale mwanandoa anapogundua kwamba ardhi au nyumba ya ndoa imewekwa rehani bila ridhaa yake***

- Taarifa itolewe haraka iwezekanavyo kwenye Halmashauri ya Kijiji na kwa Afisa Ardhi wa Wilaya aliyeko katika eneo husika, ili taratibu zifanyike za kubatilisha rehani hiyo.
- Mwanandoa husika pia anaweza kwenda mahakamani kuomba na kuweka pingamizi la rehani au rehani ibatilishwe.
- Iwapo nyumba au ardhi ya wanandoa itawekwa rehani bila idhini ya mmoja wa wanandoa anayetumia au kuishi ndani ya nyumba hiyo, rehani hiyo inakuwa batili.

***Urejeshaji wa Hakimiliki ya Ardhi***

Mtu mwenye hakimiliki ya ardhi anaruhusiwa kurejesha haki hiyo kisheria pale anapoona kwamba haihitaji tena ardhi hiyo au hana uwezo wa kuiendeleza. Mrejeshaji anatakiwa kutuma maombi ya urejeshaji kwa Kamishna wa ardhi au kwa halmashauri ya kijiji kutegemea na kundi la ardhi anayoimiliki. Sheria pia inakataza urejeshaji wa ardhi wenye nia ya kumnyima au kumdhulumu mwanandoa au mmiliki mwingine haki yake ya umiliki anayostahili au haki ya kupata maslahi katika ardhi husika. Sheria imewapa watu uhuru wa kupeleka maombi kwenye Halmashauri ya Kijiji endapo wanataka kugawa au kuhamisha haki ya kumiliki ardhi iliyopo kwenye ardhi ya kijiji. Katika kufikiria maombi ya mtu binafsi ya kutaka kutoa ardhi yake anayomiliki kihalali, Halmashauri ya Kijiji inatakiwa ihakikishe kuwa mahitaji maalum ya wanawake ya kupata ardhi yanatimizwa kwanza, ili kuhakikisha kwamba, kurejesha, kugawa au kuhamishwa kwa haki ya kumiliki ardhi hiyo hakujapangwa kwa nia ya kumdhulumu mwanamke haki yake ya kumiliki ardhi.

Kabla ya kutolewa maombi yoyote juu ya ardhi hiyo iliyorejeshwa, Halmasahuri ya Kijiji inatakiwa kwanza kumuuliza mwanandoa wa mrejeshaji kama atahitaji ardhi hiyo. Endapo mrejeshaji ni mwanaume na ana mke zaidi ya mmoja basi wake zake wataulizwa kulingana na mpangilio wa nani aliyeolewa kwanza. Vipengele vyote hivi vinampa mwanamke nafasi ya kumiliki ardhi kwa yeye kupewa ardhi hiyo kabla ardhi anayomiliki mumewe haijatolewa kwa mtu mwingine yeyote yule.

**HITIMISHO**

Kuwepo kwa Sheria hizi mpya za Ardhi kumetoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika kuomba, kutumia na kumiliki ardhi, haki ambayo kila mmoja anatakiwa kuipata kwa usawa. Kwa kuwa wanawake wana mchango mkubwa katika kutumia ardhi hasa kwenye uzalishaji mali, uhakika wa kupata ardhi utawasaidia kuinua kipato cha familia na kipato cha taifa kwa ujumla hivyo kupunguza umaskini katika nchi yetu.

Jamii pia  inajukumu la kusoma kitabu hiki kwa makini na kuelewa nafasi aliyopewa mwanamke kikatiba/kisheria juu ya kutumia na kumiliki ardhi; kwa kuelewa Katiba na sheria mwanamke anaweza kudai haki yake na mwanaume anaweza kutimiza wajibu wake kwa kutoa haki stahiki kwa mujibu wa Sheria.

# SURA YA PILI

## SEHEMU YA KWANZA

### 2.0 SHERIA YA NDOA NA HAKI YA ARDHI KWA MWANAMKE

### 2.1 MAANA YA NDOA

Ndoa ni muungano wa hiari kati ya mwanaume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao yote. Maana hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Ili ndoa ikamilike kuna vigezo vya kuzingatia kwa mujibu wa sheria ya ndoa, vigezo hivyo ni:

- Muungano huo lazima uwe wa hiari, mwanamke na mwanaume wawe wameridhia kufunga ndoa pasipo kulazimishwa.
- Muungano uwe ni kati ya mwanamke na mwanaume. Kwa maana kwamba watu wanaruhusiwa kufunga ndoa ni mwanaume na mwanamke na si watu wa jinsia moja.
- Muungano huo uwe unakusudiwa kuwa wa kudumu, wanandoa wanakusudia kukaa pamoja katika maisha yao yote.
- Wafunga ndoa wasiwe maharimu, kwa maana kwamba wanaofunga ndoa wasiwe na uhusiano wa karibu kindugu.
- Wafunga ndoa wawe wametimiza umri unaokubalika kisheria. Kwa mujibu wa sheria ya ndoa ni umri wa miaka 18 lakini hata wenye umri wa chini ya miaka 18 wanaruhusiwa ila kwa ridhaa ya wazazi/walezi au mahakama.

### 2.2 AINA ZA NDOA

Sheria ya ndoa inatambua ndoa  za aina mbili ndoa ya mke mmoja na ndoa ya mke zaidi ya mmoja ;ndoa hizi zinafungwa kwa namna tatu: yaani Kidini, Kimila na Kiserikali.

#### i. Ndoa ya Kidini

Ndoa hii hufungwa kwa mujibu wa taratibu za dini husika. Ni lazima masharti yote yatimizwe kisheria, taarifa ya nia ya kufunga ndoa itolewe, ndoa ifungwe mahali pa wazi panapokubalika kisheria na mfungishaji awe na mamlaka. Kwa mujibu wa dini ya kikristo huwa ni ndoa ya mke na mume mmoja. Lakini kwa dini ya kiislam ni ndoa ya mume na mke zaidi ya mmoja.







**ii. Ndoa ya Kiserikali**

Ndoa hii hufungwa mbele ya Mkuu wa Wilaya ambaye ndiye Msajili wa Ndoa. Ndoa itafungwa katika Ofisi ya Msajili au mahali pengine popote palipotajwa katika leseni ya kufungisha ndoa. Ndoa hizi maarufu zimekua zikifahamika kama “ndoa za bomani”

**iii. Ndoa ya Kimila**

Ndoa inaweza kufungwa kimila iwapo mmoja wa wafunga ndoa au wote wawili wanafuata sheria za mila za kabila fulani. Mdhamini wa ndoa za kimila ni Afisa Tarafa. Ndoa ya kimila hufungishwa na mtu

anayetambulika kimila kuwa ana uwezo huo. Ni muhimu sana Afisa Tarafa kuhudhuria kwenye ufungishaji huo wa ndoa kwani ndiye atakayehusika na kuleta vyeti vya ndoa kutoka kwa Msajili kwani hata ndoa hizi zinatakiwa zisajiliwe  kwenye daftari la msajili Mkuu wa ndoa. Mara nyingi ndoa hizi hazina vyeti kutokana na mazingira na miundombinu tunayoishi.

**2.3 DHANA YA KUCHUKULIA NDOA/ NDOA ZA KUFIKIRIKA**

Kuna dhana inayokanushika kuwa mwanamume na mwanamke wakiishi pamoja huweza kuchukuliwa au kufikiriwa kuwa ni mke na mume mbele ya sheria japokuwa hawakuwahi kufunga ndoa. Ili dhana hii iwepo ni lazima yafuatayo yathibitishwe.

- Lazima ithibitike kwamba mwanamke na mwanamme wameishi pamoja kwa muda wa miaka 2 au zaidi kwa mfululizo ndani ya nyumba mmoja.
- Lazima ithibitike kuwa umma unaowazunguka unawachukulia na kuwapa heshima kama mke na mume.
- Lazima ithibitishwe kuwa watu hao walikuwa na uwezo wa kuwa mke na mume wakati walipoanza kuishi pamoja na kama walikuwa na umri uliokubalika kisheria.
- Ni lazima pia ithibitishwe kuwa kati ya hao wawili au wote hakuna aliye na ndoa inayoendelea.

Mara nyingi wale wanaofunga ndoa ya kidini au kiserikali wamekuwa na fursa ya kufika mahakamani kirahisi zaidi pindi migogoro ya ndoa inapoibuka. Uzoefu unaonesha kuwa, wanawake waliofunga ndoa ya kimila ndio wapo katika matatizo makubwa ya kukosa haki zao wakati wa talaka. Mara nyingi huachana kwa kufuata taratibu za mila ambazo hufuata taratibu na tamaduni za makabila mbalimbali. Hivyo ni vigumu kupata haki stahiki wakati wa talaka.

Katika baadhi ya makabila hayana kabisa suala la mali za ndoa, kwao mwanamke akiolewa na mahari kutolewa hana kitu chochote nyumbani kwa mumewe. Hivyo wanashauriwa kwenda mahakamani pindi wanapopewa talaka kimila kwani ni jukumu la mahakama kutoa talaka na kugawa mali za ndoa. Wakati wa talaka na baadaye mgawanyo wa mali za ndoa, mwanamke anashauriwa kuomba msaada kutoka kwa mwenyekiti wa kijiji, Afisa Mtendaji wa Kijiji, diwani, kiongozi wa

dini, karani wa mahakama, asasi yoyote iliyopo kijiji au yeyote yule atakayekua na msaada.

## 2.4 HAKI NA WAJIBU KATIKA NDOA

Baada ya taratibu zote za ndoa kufuatwa na kwamba ndoa haina kasoro yoyote, mke ana haki mbalimbali anazostahili kuzipata kisheria. Haki hizo ni kama ifuatavyo:-

### 2.4.1 Matunzo

Mke au wake wana haki ya kutunzwa na mume wao kwa kuwapatia mahitaji muhimu kama chakula, malazi,mavazi, matibabu na n.k kulingana na uwezo alionao mwanaume.

Kama ni kijijini mume anapaswa kumwonyesha mkewe mahali pa kulima na kumsaidia kukata miti na visiki. Iwapo mume ana mke zaidi ya mmoja ana wajibu wa kuwatunza wote bila ya upendeleo. Pia mume ana wajibu wa kuwatunza watoto wote waliozaliwa ndani ya ndoa.

### 2.4.2 Kumiliki Mali

Mke ana haki ya kumiliki mali aliyoipata kabla ya ndoa na hata wakati wa ndoa kama ameipata kwa fedha zake mwenyewe au kupewa zawadi. Mke pia ana haki ya kuingia mikataba, kufungua madai dhidi ya wadeni wake au kudaiwa, kununua mali au kuiuza. Kwa kuwa mume nae ana haki hizo hizo, hii inamaanisha kuwa ndoa peke yake haibadilishi haki ya kumiliki mali kati ya mke na mume. Pamoja na hali hii mke na mume wanaweza kukubaliana kuwa mali ambazo kila mmoja alikuwa nazo kabla ya ndoa au wakati wa ndoa ziwe zao kwa pamoja.

### 2.4.3 Mke kukopa kwa dhamana ya mumewe

Kwa kuwa katika hali ya kawaida mume ana wajibu wa kumtunza mke na watoto kuna wakati inawezekana mume akasafiri kwa muda mrefu na hakuacha fedha au alizoacha zimekwisha, au mume amemtoroka mke na kumwachia watoto. Mke ana haki ya kukopa fedha kwa jina la mumewe au kuweka rehani mali ya mumewe. Mke ana uwezo wa kutumia mali ya mumewe ambayo inahamishika au kutumia fedha za mumewe zilizoko mikononi mwake kwa ajili ya kununulia mahitaji ya muhimu kwa ajili yake na watoto wake ni halali kisheria.

Haki hizi zinakuwepo kama mke na mume wanaishi pamoja au kama wametengana kwa mapatano kuwa mume atatoa matunzo na mume amepuuzia mapatano hayo. Jambo la kuzingatia kwa makini hapa ni kuwa ili haki ya kutumia mali ya mume iweze kuwapo ni lazima mahitaji yanayonunuliwa yawe ni yale ambayo kama mume mwenyewe angekuwepo angekuwa na uwezo wa kuyanunua kulingana na pato lake.

**2.4.4 Haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa**

Nyumba ya ndoa ni nyumba ambayo mume na mke wanaishi wakati wa ndoa. Hata kama wana nyumba nyingi ni nyumba moja tu ndiyo inayochukuliwa kama nyumba ya ndoa. Pamoja na kuwa nyumba ya ndoa inaweza kuwa mali binafsi ya mke au mume, nyumba hiyo haiwezi kuuzwa, kuwekwa rehani au kuchukuliwa na mtu mwingine kama zawadi bila ya makubaliano ya wote wawili.

Ikiwa mume atafanya chochote kwenye nyumba hii bila ya makubaliano na mke, mke atakuwa na haki ya kuishi katika nyumba hiyo hadi hapo Mahakama itakapotoa maamuzi ya kuvunja ndoa hiyo, kutengana au amri ya matunzo. Kadhalika mume naye anayo haki hiyo hiyo iwapo mke ndiye mwenye nyumba na anataka kumfukuza mumewe. Ikumbukwe kuwa nyumba ya ndoa siyo lazima iwe nyumba ambayo mmoja wao amenunua ama amejenga. Hata kama nyumba ni ya kupanga bado itatambulika kisheria kama nyumba ya ndoa.

**2.4.5 Mali iliyopatikana wakati wa ndoa**

Mali ya mke au mume iliyopatikana kutokana na jasho lao wote wawili ni mali yao kwa  pamoja hata kama juhudi zao au jasho lao katika kupata mali hizi si sawasawa. Lakini pamoja na hayo kuna dhana inayokanushika kuwa kama mali hii imeandikishwa kwa jina la mmoja wao basi ni mali yake. Ni wajibu wa yule anayedai kuthibitisha kuwa ni mali ya pamoja na kwamba mali imeandikishwa kwa jina la mwenzi wake.

## 2.5 HAKI YA ARDHI YA  MWANAMKE WAKATI WA TALAKA

**Maana ya talaka**

Talaka ni amri ya mahakama inayotolewa kuonesha kuwa ndoa imevunjika katika kiwango cha kutotengenezeka. Hii inamaanisha

kuwa wanandoa hawawezi kuishi tena kama mume na mke.

Baada ya mahakama kutoa talaka itaamuru kugawanywa kwa mali za familia ambazo wanafamilia walishiriki katika kuzipata kwa pamoja, mali ambazo si za familia hazitahusishwa kwenye mgao huo. Kwa sasa, mahakama inazingatia pia mchango wa mwanamke alizoweka katika kupata mali ya familia. Mchango wa mwanamke unajumuisha kazi za nyumbani za kuhudumia familia kwa mfano kufua, kupika kuhudumia watoto na n.k, hii ni kwa wale wanawake ambao si wafanyakazi au wafanyabiashara.

## 2.6 KUTENGANA KWA TALAKA

Kutengana kwa talaka ni haki alizonazo kila mwanandoa endapo ndoa yao itakuwa na matatizo kiasi cha kupelekea wanandoa wasindwe kuishi pamoja. Kutengana ni hali ya wanandoa kuacha kuishi pamoja katika nyumba moja chini ya dari moja.

### AINA ZA KUTENGANA

**Kutengana kupo kwa aina mbili:**

1. Kwa hiari ya wanandoa wenyewe
2. Kwa amri ya mahakama

Amri ya kutengana kama ilivyoelezwa katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaeleza kuwa talaka inapotolewa na mahakama inawafanya wanandoa wasikae pamoja lakini haiondoi wajibu na majukumu alionayo mwanandoa kuhusiana na matunzo.

Kwa mujibu wa kifungo cha 100 cha Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 mahakama haiwezi kusikiliza shauri la talaka kama ndoa haijadumu kwa miaka miwili. Ili shauri la talaka lipokelewe kabla ya miaka miwili ya ndoa ni lazima mahakama itoe idhini. Idhini hiyo inatolewa pale tu inapothibitishwa mwanandoa anapata mateso yasiyo ya kawaida.

## 2.7 SABABU ZA MAHAKAMA KUTOA TALAKA

Sheria ya Ndoa imeainisha sababau mbalimbali zinazopelekea mahakama kutoa talaka kama ifuatavyo:

- Ugoni na hasa kama tabia hiyo inaendelea hata baada ya mwanandoa mwingine kupinga tabia hiyo.
- Ukatili wa kiakili au wa kimwili ambao anatendewa mwanandoa mmoja au kwa watoto.

- Kuzaa nje ya ndoa.
- Kubadilisha dini tofauti na dini ya mwanzo.
- Ulawiti.
- Kuzembea wajibu kwa makusudi.
- Kutelekeza familia kwa muda wa miaka mitatu.
- Kichaa kisichopona.
- Kipigo.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.8 MAMBO YA MSINGI KATIKA URITHI WA MALI YA FAMILIA

Uzoefu umeonesha kuwa, kuwepo kwa matatizo mengi katika familia au koo pale mtu anapofariki. Matatizo hayo hutokana na utata na kutokujua taratibu za kusimamia na kugawa mirathi kwa wahusika, pia mara nyingi mila na desturi zimekua zikimgandamiza mwanamke katika kupata mali za marehemu.

## 2.9. MAANA YA MIRATHI

Mirathi ni utaratibu wa namna mali ya marehemu itakavyogawiwa kwa warithi wake. Mgawanyo wa mirathi nchini unaongozwa na sheria tatu za mirathi ambazo ni; *Sheria ya Kimila, Sheria ya Kiislam*, na *Sheria ya Kiserikali.* Pamoja na sheria hizo, sheria ya mtoto ya mwaka 2009 imeeleza kuwa mtu yeyote hatakuwa na haki na uwezo wa kumnyima mtoto haki ya kurithi mali za wazazi wake.

## 2.10.1 SHERIA ZA KIMILA

Watumiaji wa Sheria za Kimila ni Watanzania wote wazawa, wasio na asili ya Kiasia, Kizungu au Kisomali, endapo itadhihirika kuwa mzawa huyu aliacha kabisa mila na desturi za kabila lake, mahakama inaweza kutumia Sheria ya Kiserikali au Sheria ya Kiislamu kama marehemu alikuwa Muislamu katika kushughulikia mirathi yake.

## 2.10.2 URITHI KATIKA SHERIA ZA KIMILA

Katika sheria za kimila, kama marehemu ameacha watoto, huwa ndio warithi wakuu wa mali za marehemu. Urithi katika sheria hizi umegawanywa katika madaraja matatu.

**Daraja la Kwanza**
Mrithi wa kwanza ni mtoto wa kiume wa kwanza wa ndoa. Kama marehemu alikuwa na ndoa ya wake wengi, daraja la kwanza ni mtoto wa kiume wa mke mkubwa wa ndoa. Kama mke mkubwa hana mtoto wa kiume basi daraja la kwanza litaenda kwa mtoto wa kiume alietangulia kuzaliwa. Huyu hurithi sehemu kubwa kuliko warithi wote.



**Daraja la Pili**
Daraja hili linajumuisha watoto wote wa kiume waliosalia, ambao hurithi sehemu kubwa kuliko watoto wa kike ambao ni daraja la tatu.



**Daraja la tatu**
Ni watoto wote wa kike bila kujali umri wao au nafasi yao ya kuzaliwa. Hawa hupata sehemu ndogo kuliko wote. Kama hakuna watoto wakiume, watoto wa kike hupewa urithi zaidi.



Katika kanuni hizo imewekwa bayana kwamba watoto wa kike hawaruhusiwi kurithi ardhi ya ukoo wala kuiuza bali wanaruhusiwa kuitumia tu mpaka watakapoolewa au kufa.

Ni wazi kuwa kwa sheria za kimila ni za ubaguzi na kandamizi kwani zinampa mwanamke nafasi ndogo sana ya kurithi mali za familia. Hivyo sheria hizo zinakinzana na sheria za ardhi na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazosisitiza usawa katika kumiliki mali. Katiba ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania inaeleza kuwa sheria yoyote inayombagua mtu yeyote ni batili.

**2.10.3 WATOTO WALIOZALIWA NJE YA NDOA**
Watoto waliozaliwa nje ya ndoa hawaruhusiwi kurithi mali za baba, wanaweza kurithi tu kama wamehalalishwa kwa kufuata desturi au taratibu zinazojulikana na kutambulika katika jamii hiyo. Pia hata kama wamehalalishwa kwa mila na desturi husika hawawezi kurithi mali katika daraja la kwanza kama kuna mtoto wa kiume ndani ya familia.

**2.11 MJANE**
Mjane hakutajwa katika madaraja ya urithi ingawa ni wazi kwamba

mke ndiye mvujajasho zaidi katika familia. Kwa mujibu wa sheria hiyo ya kimila, mjane inabidi aishi kwa kutegemea watoto wake ambao watarithi mali ya mume wake.

Iwapo marehemu hakuacha watoto wala wajukuu, kaka na dada zake waliochangia baba na mama ndio warithi. Kaka wa kwanza atakuwa ni daraja la kwanza ambaye atapata sehemu kubwa. Kaka waliobaki watakuwa daraja la pili ambao watapata sehemu kubwa kuliko daraja la tatuna dada wote watakuwa katika daraja la tatu.

Ikiwa marehemu hakuacha kaka wala dada, basi mali hiyo yaweza kurithiwa na watoto wa kaka au dada zake kama wapo. Kama wote hawapo, baba wa marehemu anaweza akarithi. Na iwapo baba hayupo, baba wadogo watarithi na kama hawapo shangazi atarithi, kama naye hayupo ndugu wengine watarithi. Kazi za warithi siku zote inasemekana ni kutunza mjane/wajane na kuwagawia asilimia kidogo sana ya mali inayohamishika. Kama ndugu wa kurithi hawapo basi mali za marehemu zitapelekwa serikalini.

**2.12 MJANE ASIYE NA MTOTO**

Kama mjane hana watoto , Sheria inasema mali ya marehemu itagawanywa nusu na mjane hupewa 1/20 ya nusu ya mali ya marehemu. Pia mjane ana haki ya kuishi katika nyumba ya ndoa hadi atakapoolewa au kufariki.

Katika sheria ya Kimila mjane haruhusiwi kurithi mali za marehemu mume wake, sheria hiyo inasema kuwa mjane mwenye watoto inabidi aishi kwa kutegemea watoto wake. Mjane ambaye hana watoto atabaki katika nyumba ya marehemu na kupewa asilimia 20 ya nusu ya mali ya marehemu mume wake na kuitumia wakati wa uhai wake. Akifariki au kuolewa na mtu mwingine nje ya ukoo mali hiyo na nyumba aliyokua anakaa itagawiwa kwa warithi halali wa marehemu. Sheria hii pia inasema mume hawezi kurithi mali ya marehemu mkewe katika urithi usio na wosia, isipokua pale tu ambapo mke hakuacha watoto na hakuacha kabisa mtu katika ukoo wake. Sheria hii kwa sasa inakosa uhalali wa kikatiba kwa kuwa haki za binadamu zinataka usawa bila ubaguzi.

## 2.13 SHERIA YA KIISLAM

Sheria ya Kiislam inatumika kugawa mirathi kwa watanzania wote ambao itathibitika kuwa wameacha mila na desturi zao na ambao Uislamu huwaongoza katika vipengele vyote vya maisha yao pamoja na watu wale ambao si wazawa ila ni waislamu.

**Mgawanyo wa mirathi kwa sheria za kiislam.**

1. Mjane/wajane kama kuna watoto anarithi moja ya nane (1/8) ya mali ya marehemu
2. Mjane/Wajane kama hakuna watoto anarithi robo (1/4) ya mali
3. Wazazi wa marehemu hupewa 1/6 ya salio baada ya kuondoa fungu la mjane/wajane

Katika sheria ya Kiislamu, marehemu anaruhusiwa kuacha wosia kwa theluthi moja tu (1/3) ya mali yake kwa amtakaye. Theluthi mbili (2/3) ya mali yake lazima ifuate utaratibu wa Sheria za Kiislamu yaani irithiwe na warithi wake. Kwa maana hiyo wosia ulioachwa na marehemu kwa Zaidi ya theluthi moja(1/3), bila ridhaa ya warithi halali wa marehemu ni batili kwa sheria ya kiislam.

## 2.14 SHERIA YA KISERIKALI

Sheria hii ilitungwa huko India mwaka 1865 na ikahalalishwa kutumika hapa Tanzania toka enzi ya utawala wa Waingereza.Sheria ya Kiserikali hutumika kwa Watanzania walioacha mila na desturi pamoja na watu wengine ambao si wazawa.

Mgawo wa urithi katika Sheria ya Kiserikali

Iwapo marehemu ameacha watoto;

- Mjane/ wajane hupewa moja ya tatu (1/3) ya mali hurithiwa na mjane/wajane.
- Watoto wote waliobaki hugawiwa mbili ya tatu (2/3) sawa kwa wote.

Kama hakuna watoto mali hugawiwa ifuatavyo;

- Mjane/ mgane hupata nusu (½) ya mali ya marehemu
- Wazazi wa marehemu au ndugu wa marehemu iwapo wazazi hawapo hupata nusu ya mali (½) ya marehemu.

## 2.15 MAHALI PA KUFUNGUA KESI ZA MIRATHI

Kesi zinazohusu kugawa mali ya marehemu kwa Sheria za Kimila, na ya Kiislam, lazima zifunguliwe Mahakama za Mwanzo na sio Mahakama nyingine zozote. Mahakama za Wilaya/Hakimu Mkazi na Mahakama Kuu hushughulikia tu mirathi ya marehemu pale ambapo Sheria ya Kiserikali hutumika.




## SEHEMU YA TATU

## 2.16 WOSIA

### Maana ya Wosia

Wosia ni kauli inayotolewa na mtu wakati wa uhai wake kwa hiari yake kuonyesha nia yake jinsi gani angependa mali zake zigawanywe baada ya kufa kwake.

### Aina za wosia

i. Wosia wa maandishi
ii. Wasia wa mdomo.

### 2.16.1 WOSIA WA MAANDISHI

Kwa mtu anayejua kusoma na kuandika, lazima atoe wosia katika

maandishi. Wosia unatakiwa uandikwe kwa kalamu ya wino usiofutika au upigwe chapa. Tarehe ya kutoa wosia ni muhimu. Kwa mtoa wosia anaejua kusoma na kuandika wanatakiwa mashahidi wawili watakao weka saini zao kuthibitisha wosia huo. Kwa mtu asiyejua kusoma na kuandika wosia wake pia unaweza kuandikwa ila sharti kuwe na mashahidi wanne wawe ni watu wanaojua kusoma na kuandika.

Wosia unatakiwa kusainiwa na mtu alieutoa, na kama mtu hajui kusoma na kuandika aweke alama ya kidole gumba mbele ya mashahidi wake. Wosia unaweza kueleza msimamizi wa mirathi ambao mtoaji wa wosia angependa wasimamie ugawaji wa mali zake. Wosia unaweza kubadilishwa kwa kufuata taratibu za kisheria kwani hutumika pale tu mtu anapofariki.

### 2.16.2 WOSIA WA MDOMO

Wosia huu unatolewa na mtu asiyejua kusoma na kuandika, pia unapaswa ushuhudiwe na mashahidi wasiopungua wanne. Ambao wawili kati yao lazima wawe wana ukoo wa mtoa wosia. Wosia huo waweza kufutwa kwa kutoa wasia mwingine wa mdomo au kwa kutoa wosia wa maandishi mbele ya mashahidi.



## 2.17 WOSIA KATIKA SHERIA ZA KIMILA

Wosia wa kimila lazima uwe na mashahidi wasiopungua wanne ambao huchaguliwa na mtoa wosia mwenyewe. Mashahidi wote wanatakiwa washuhudie kwa wakati mmoja. Warithi hawapaswi kuwa mashahidi, iwapo wamekuwa mashahidi wosia huo utakuwa ni batili, yaani utakosa nguvu za kisheria. Wosia ni siri itakayofichuliwa pindi mtoa wosia atkapofariki. Mara nyingi wosia wa kimila hutolewa kwa mdomo.

## 2.18 WOSIA KATIKA SHERIA ZA KISERIKALI

Hakuna tofauti kubwa na wosia katika Sheria za Kimila bali wosia huu unapaswa kuwa katika maandishi. Hivyo vipengele vyote vya wosia wa maandishi vinatumika. Mwosia anaweza kufuta au kuongeza maneno mengine kwa kuandika maandishi mengine ambayo itabidi yazingatie masharti ya uandikaji wa wosia. Wosia wa maandishi unatakiwa uwandike kwa kalamu ya wino isiyofutika au upigwe chapa. Tarehe ya siku kutoa wosia ni muhimu. Kwa mtoa wosia anayejua kusoma na kuandika wanatakiwa mashahidi wawili watakao weka saini zao kuthibitisha wosia huo.

## 2.19 WOSIA KATIKA SHERIA YA KIISLAMU

Kwa mujibu wa Sheria ya Kiislamu, mtoa wosia/mwosia haruhusiwi kuusia mali yake yote. Huruhusiwa kuusia 1/3 tu ya mali yake, akitaka kuusia zaidi ya hapo hana budi kupata ridhaa ya warithi halali wa mtoa wosia. Sehemu 2/3 ni lazima ifuate taratibu za kiislamu za ugawaji mali ya urithi.

## 2.20 NAMNA YA KUHIFADHI WOSIA

Wosia unaweza kuhifadhiwa sehemu yoyote yenye usalama kuepusha uwezekano wa kufanyiwa mabadiliko na mtu asiye mwosia. Hivyo, wosia waweza kutunzwa mahakamani, msikitini, kanisani, kwa mwanasheria au katika Taasisi za Kifedha




## 2.21 TARATIBU ZA KUFUNGUA MIRATHI

Wosia ukiwepo;

1. Mtu anapofariki, kifo kiandikishwe katika ofisi ya vizazi na vifo katika wilaya husika ndani ya muda wa siku 30 tangu kifo kutokea.
2. Endapo wosia haukumtaja msimamizi wa mirathi japokuwa si utaratibu wa kisheria mkutano wa ukoo/familia ufanyike na kupendekeza msimamizi wa mirathi.
3. Msimamizi aliyependekezwa au kutajwa katika wosia afungue mirathi katika mahakama ya mwanzo iwapo sheria itakayotumika ni ya kimila au ya kiislam akiwa na nakala ya muhtasari wa kumbukumbu za kikao cha ukoo na cheti cha kifo.
4. Ukoo au ndugu wa marehemu hutoa mapendekezo tu juu ya mtu anayefaa kuwa msimamizi wa mirathi lakini ni mahakama pekee yenye uamuzi wa mwisho pale wosia haukusema nani atakuwa msimamizi wa mirathi.

Wosia usipokuwepo;

1. Mtu anapofariki, kifo kiandikishwe katika ofisi ya vizazi na vifo katika wilaya husika ndani ya muda wa siku 30 tangu kifo kutokea.

2. Mkutano wa ukoo/familia ufanyike kumpendekeza msimamizi.
3. Msimamizi aliyependekezwa aende kufungua mirathi mahakamani akiwa na nakala ya muhtasari wa kumbukumbu za kikao cha ukoo na cheti cha kifo.
4. Mahakama hutoa tangazo la mirathi kwa muda wa siku 90 kama hakuna pingamizi lolote msimamzi hukabidhiwa barua za usimamizi wa mirathi.
5. Msimamizi anatakiwa kugawa mirathi kwa mujibu wa sheria, kufuatana na maisha aliyoishi marehemu.




**HITIMISHO**

Ni wazi kuwa moja ya changamoto katika sheria za mirathi ni namna mwanamke anavyobaguliwa na sheria za kimila katika kurithi mali za familia ikiwa ni wazi kwamba mwanamke ndiye mwenye mchango mkubwa katika kupata mali za familia. Serikali pia inatakiwa kuanagalia sheria hizi za kimila na kuzifanyia marekebisho ili ziendani na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosisitiza katika usawa.

# SURA YA TATU

## 3.0 USHIRIKI WA WANAWAKE KATIKA MASUALA YA ARDHI

Sheria za Ardhi za mwaka 1999 zimeweka mfumo bora wa utawala ambao unawawezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika masuala ya ardhi na kuwakilishwa katika mipango na maamuzi yanayohusu ardhi. Kwenye usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya ardhi, wanawake pia wanapaswa kushiriki kwenye kamati za usuluhishi katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo

## 3.1. BARAZA LA TAIFA LA USHAURI LA ARDHI

Baraza hili linaundwa chini ya kifungu 17 cha Sheria ya Ardhi Namba 4 ya mwaka 1999. Baraza hili linatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua saba (7) na wasiozidi kumi na mmoja (11). Wajumbe hawa wanateuliwa na Waziri wa Ardhi. Jukumu kubwa la baraza hili ni kupitia na kuangalia upya masuala ya ardhi na kumshauri waziri juu ya sera ya Taifa ya ardhi kwa nia ya kufanya marekebisho na mabadiliko inapobidi, ili kuboresha utekelezaji wa masuala ya ardhi nchini. Sheria imemtaka waziri katika kuteua wajumbe hao azingatie uwiano unaoridhisha baina ya wajumbe wanawake na wanaume.

## 3.2 KAMATI YA UAMUZI YA KIJIJI

Hii ni kamati ambayo inaweza kuundwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji chini ya kifungu cha 53 cha Sheria ya Ardhi ya Vijiji Namba 5 ya mwaka 1999, kwa ajili ya kusuluhisha migogoro inayohusiana na mipaka ya ardhi, haki ya njia, maslahi ya wanawake, walemavu, na watu wasiokuwepo kijijini.

Kamati hii inaundwa na wajumbe wasiozidi tisa (9), ambapo wajumbe wasiopungua wanne (4) wanatakiwa wawe wanawake. Wajumbe wa kamati hii watatumikia kwa kipindi cha miaka mitatu (3) na wataweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu.

Kikao halali cha Kamati ya Uamuzi ya Kijiji kinatakiwa kuwa na wajumbe wasiopungua watano (5), ambao wawili (2) kati yao ni lazima wawe wanawake. Mtu yeyote ambaye hakuridhika na uamuzi wa Kamati ya Uamuzi ya Kijiji anaweza kukata rufani dhidi ya uamuzi huo

kwenye Baraza la Ardhi la Kijiji ndani ya kipindi cha siku thelathini (30) baada ya kutolewa kwa uwamuzi.

Katika utawala na usimamizi wa ardhi ya kijiji; Sheria ya Ardhi ya Vijiji, imeipa mamlaka kamati hii, wajibu wa kutambua ardhi ya kijiji na mipaka yake, kutenga na kuweka mipaka yake na kutoa njia na haki zingine za kutumia njia ambazo itaziona ni muhimu kwa umiliki bora wa ardhi. Pia inajukumu la kulinda maslahi ya wanawake, watoto, walemavu na wanakijiji wasiokuwepo kijijini ila wana maslahi ya ardhi kijijini.

### 3.3 BARAZA LA KATA

Wanawake pia wamepewa nafasi ya uwakilishi katika baraza la Kata, kwa mujibu wa sheria ya Mabaraza ya Kata, Baraza la Kata litakuwa na wajumbe wasiozidi wanane ( 8 ) na wasiopungua wanne ( 4 ), na kati yao, wajumbe watatu lazima wawe ni wanawake.

### 3,4 BARAZA LA ARDHI LA KIJIJI

Baraza la Ardhi la Kijiji ambalo lina kazi ya kusuluhisha na kutatua migogoro yote ya ardhi kijijini. Baraza la Ardhi la Kijiji linatakiwa kuwa na wajumbe saba (7) ambapo watatu (3) kati yao ni lazima wawe wanawake. Wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji wanateuliwa na Halmashauri ya Kijiji na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Kijiji.Kikao halali cha Baraza la Ardhi la Kijiji kinatakiwa kiwe na wajumbe wane (4) ambapo wawili (2) kati yao ni lazima wawe wanawake.Baraza la Ardhi la Kijiji linatakiwa kufanya kazi zake kwa kuzingatia misingi ya kimila ya usuluhishi pamoja na misingi ya haki na usawa.

Pamoja na uwakilishi wa wanawake katika vyombo mabalimbali vya usuluhishi wa migogoro ya ardhi, pia wanawake wanasisitizwa kuhudhuria mikutano yote ya vijiji inayoitishwa, kwani mikutano hii ndio jukwaa la maamuzi ya pamoja juu ya usimamizi na mgawanyo wa rasilimali za kijiji. Hivyo ni jukumu la wanakijiji wote hasa wanawake kuhudhuria mikutano hiyo ili waweze kupaza sauti zao na kushiriki katika kutoa maamuzi ya rasilimali za kijiji.

### HITIMISHO

Wanawake ni watumiaji wakuu wa ardhi hivyo vyombo vinavyohusika na masuala ya usimamizi na utawala wa ardhi vihakikishe kuwa wanawake na wanaume wanashirikishwa ipasavyo katika masuala

yahusuyo ardhi.

Wanawake wahakikishe kuwa wanazitumia nafasi wanakazokuwanazo kwa kushiriki na kutoa mawazo yao kwa lengo la kuboresha maslahi ya familia zao na taifa kwa ujumla.

PELUM Tanzania
S.L.P 390, Morogoro-Tanzania
Simu/Nukushi: +255 23 2613677
Barua pepe: info@pelumtanzania.org
Tovuti: www.pelumtanzania.org